BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Pili – Tarehe 16 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

24. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

    Utabiri mbali mbali unaonesha wazi kuwa nchi yetu ya Tanzania itakabiliwa na mvua kubwa zinazotarajiwa kunyesha hivi karibuni.

Je, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejipanga vipi kuwasaidia na kuwanusuru wananchi wanaokumbwa na maafa ya mvua hizo yanayotokea katika sehemu mbali mbali.

## Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

104. MHE. DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali huwaongeza mishahara wafanyakazi wake pale hali ya uchumi inaporuhusu lakini katika kuongezwa huko hujitokeza changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na kusahauliwa kuongezwa na kukosewa mishahara ya baadhi ya watumishi. Kutokanana na makoseo hayo Serikali huwalipa 'Arears' wafanyakazi hao ili kusahihisha makosa yaliyofanyika.

(a) Je, takwimu zinaonesha ni idadi ya wafanyakazi wangapi ambao mishahara yao ilikosewa tangu kuanza kwa kiwango kipya cha ulipaji wa mishahara na ni hatua gani zilichukuliwa na Serikali.

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho Serikali inadaiwa kutokana na makosa haya ya mishahara.

(c) Kwa kuwa kuna wafanyakazi waliostaafu wakati mishahara yao ikiwa imekosewa, Je, Serikali katika kutoa mafao ya uzeeni na pensheni kwa wafanyakazi hawa, hutumia mishahara iliyorekebishwa au ile iliyokosewa.

## Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

36. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Katika Bajeti iliyopita ya mwaka wa fedha 2023, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango alisema kuwa Gawio la Zanzibar linalotokana na misaada ya kibajeti kutoka nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo (GBS) limeongezeka kutoka 4.5% hadi kufikia 9.0%.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha ambacho Zanzibar imepokea kwa mwaka huo wa fedha (2023).

(b) Na kama Zanzibar haijapokea fedha hadi sasa, ni nini kimekwamisha.

88. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali imeweka pensheni kwa wastaafu ili kuwapunguzia ugumu wa maisha na kuwapatia stahiki zao.

Kwa nini baadhi ya wastaafu walilipwa pensheni zao na baadhi yao hawakulipwa hadi hii leo.

## Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

38. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kumekuwa na changamoto kubwa ya vifo na ulemavu kwa madereva wa bodaboda, kutokana na uendeshaji wao usiofuata sheria na fujo.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani madhubuti kwa waendesha bodaboda wanaokiuka Sheria ya Usalama Barabarani.

(b) Je, Serikali imejipanga vipi kunusuru vifo na ulemavu kwa madereva wa vyombo hivyo.

## Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

3. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Changamoto ya uvujaji wa skuli ya Kitogani inawalazimisha wanafunzi wa skuli hiyo, kuakhirisha masomo wakati wa mvua zinaponyesha.

(a) Je, Wizara yako imewahi kuifahamu changamoto hiyo.

(b) Je, ni lini skuli hiyo itafanyiwa ukarabati.

(c) Je, Serikali inawaelekeza nini wananchi wa shehia ya

Kitogani.

63. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Chekechea iliyopo katika shehia ya Kilimani Tazari inakumbwa na changamoto ya kuvuja hasa katika banda wanalosomea wanafunzi. Hali hii huwalazimu walimu kuwarejesha majumbani mwao wanafunzi hao wakati mvua inaponyesha.

(a) Je, ni lini banda wanalosomea wanafunzi hao litafanyiwa ukarabati na kuezekwa.

(b) Je, Serikali inatoa kauli gani kwa wananchi na walimu wa skuli hiyo.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

7. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Visiwa vya Kokota, Funzi na Mtambwe Mkuu ni visiwa vinavyopatikana katika jimbo la Mtambwe ambavyo kwa kiasi kikubwa vilikuwa vikiitegemea hosptiali ya Wete kwa huduma za afya ikiwemo huduma ya mama na mtoto. Hata hivyo, kuhamishwa kwa hospitali ya Wete kwenda Kinyasini kumeleta usumbufu mkubwa kwa wakaazi wa visiwa hivi.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo vya afya katika visiwa hivi ili kupunguza usumbufu kwa wananchi wanaohitaji huduma za afya na wanaolazimika kusafiri kwa masaa mengi kufuata matibabu Kinyasini.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuweka gari ya dharura katika hospitali ya Wete ili kuwasaidia wagonjwa walio katika hali mbaya kuwafikisha haraka katika hospitali ya Kinyasini hususani wanaotokea katika visiwa.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

4. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

   Vyombo vya Habari vya umma vikiwemo Gazeti la Zanzibar Leo, ZBC Radio na ZBC TV vinastahili pongezi kwa kuuhabarisha umma. Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kwamba asilimia kubwa ya habari na taarifa zinazotolewa na vyombo hivyo vinaonyesha zaidi taarifa na matukio ya viongozi wa chama tawala na sio kwa viongozi wa vyama vingine.

   (a) Je, Serikali haioni kwamba kutoa taarifa za viongozi wa chama tawala peke yake ni kuwanyima wananchi haki yao ya kupata taarifa na kuvinyima Vyombo vyetu uhuru wa kujiendesha kibiashara.

   (b) Je, ni mambo gani yanavitafautisha vyombo vya Habari vya Serikali na vile vya vyama vya siasa.

   (c) Je, kwa miaka mitatu iliyopita (2020/2021 – 2022/2023), ni matukio mangapi mubashara yamerushwa na ZBC Radio na ZBC TV yakihusisha chama tawala na yakihusisha vyama vyengine.

**<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:</u>**

74. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

   Tunalipongeza Shirika la ZSTC la Zanzibar kwa kuwa na Tawi lake la kuendeleza biashara ya karafuu hapo Dar es Salaam. Hata hivyo, kuna taarifa kuwa Mikoa wa Morogoro na Tanga inazalisha kwa kiwango kikubwa karafuu, jambo ambalo linaweza kuleta mgongano wa kimaslahi ya kibiashara.

   (a) Je, kuna ukweli wowote wa taarifa hii.

   (b) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kuwa biashara yetu hii inaendelea kuimarika hapa Zanzibar.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2024/2025.

Zanzibar,
16 Mei, 2024.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA